

TUNAKWENDA WAPI BAADA YA KIFO

Yohana 14:1-35

Msifadhaike mioyoni mwenu; mnamwamini Mungu niaminini na mimi. Nyumbani mwa Baba yangu mna makao mengi; kama sivyo, ningaliwaambia: maana naenda kuwaandalia mahali. Basi mimi nikienda na kuwaandalia mahali. Nitakuja tena niwakaribishe kwangu: ili nilipo mimi nanyi muwepo.

Acha tusikie kile Nabii wa Mungu amesema juu ya hilo:

Yesu alisema na kwenda kuwaandalia mahali, ili nilipo mimi nanyi muwepo, hivyo basi, Yesu anawaambia wanafunzi kwamba maisha hayaishii katika kifo.

Sasa, kwa kusoma hii lilikuwa somo la mazishi, kifo kimewekwa tu mbele yetu, na hatujui kama.... labda kunaweza kuwepo na baadhi humu jengoni usiku hawata toka nje hapa wakiwa hai katika maisha haya ya kimwili. Hivyo ndivyo jinsi lisivyo na uhakika Dakika tano kutoka sasa inaweza kuwa kwamba kijana, mwenye afya, vijana katika jengo hili wanaweza kuwa maiti, dakika tano kutoka sasa. Tungeliweza kuwa utukufuni kila mmoja wetu. Hatujui tu hilo liko mikononi kwa Mungu Yesu alisema hajui Yeye mwenyewe wakati huo ungelikuwa. Lakini hilo lilikuwa mikononi mwa Baba pekee.

Sasa, lakini alikuwa akiwaambia kwamba kuna uhai baada ya kifo. Kwa sababu naenda kuwaandalia mahali ambapo atawapokea, ikionyesha kwamba kuna (alikuwa akiwaambia) kwamba kulikuwa na uhai baada ya maisha haya kwisha. Na nifaraja jinsi gani ambayo ingelipaswa kutupa sisi sote kujua kwamba baada ya maisha haya kwisha kuna maisha ambayo tunayaandea na kama unavyozeeka hilo linakuwa halisi zaidi kwako. Kama unavyo-anza kuona siku za uhai wako zikisogea karibu, kisha unaanza kujiweka karibu zaidi ukijiweka tayari kwa tukio hilo. Ni mwendelezo wa maisha yale yale katika dunia nyingine, mahali pengine

Sasa unaona, hakuna tofauti yoyote ikiwa unaishi au unakufa utatoka. Vyovyote vile, kwamba kufa, si lolote kwa Mkristo yeye kwa vyovyote hafi.

Acha tusome Yohana 11:25-26

Yesu akamwambia mimi ndio huo ufufuo na uzima, yeye aniaminie mimi ajapokufa atakuwa anaishi: na kuniadini hata kufa kabisa hata milele je! Unayasadiki hayo?

Unapokufa mwili wako, hufa. Neno lile mauti maana yake ni “kutengana”. Kutenganishwa tu na wapendwa wenu. Lakini hapa yeye ataka hili katika Yohana 5.24. Yeye alisikiaye neno langu na kumwamini yeye aliyenipeleka yuna uzima wa milele wala halingii hukumuni bali amepita kutoka mautini kuingia uzamani.

Sasa watu wengi wa-Adventisti wanaamini kuwa mtu anapokufa yeye huingia na kukaa kule. Nafsi. Mwili na kadhalika mpaka siku ya kiamu na wao..... wanaita hilo “kulala kwa nafsi”. Hilo ni sawa ni zuri mradi tu wamemwamini Yesu Kristo na wamezaliwa mara ya pili hilo halitawadhuru lakini sasa kulingana na maandiko mtu afapo. Kama yeye ni mkristo, kama yeye amezaliwa mara ya pili, amejazwa na Roho Mtakatifu haitampasa kamwe kusiimama katika hukumu ya Mungu. Ona? Yeye aenda moja kwa moja katika uwepo wa Mungu. Naye hata hukumiwa kamwe kwa sababu amekwisha..... ona? (Wafilipi 1:21-23) (Warumi 8:1-2). Haiwapasi kusimama kwa ajili ya yale Kristo.... jambo lote ndilo hili katika maneno machache: Mungu alisema, siku utakayokula hayo, utakufa. (Mwanzo 2:15-17) hilo latosha.

Sasa, Mungu hana budi kutimiza Neno lake, Yeye hawezi kufanya lingine ila kutumia Neno lake. Kwa sababu yeye ni Mungu. Vema basi, yeye hawezi. Ndipo, yeye... umetengwa na Mungu. Ila ... ndiposa umezaliwa katika dhambi, ukaumbika katika uovu, ukaja ulimwenguni ukinena uongo. (Isaya 64:6). Kwa hiyo ulipozaliwa asili yako ni mwenye dhambi, kwa hiyo hakuna lolote kamwe uwezalo kufanya juu yake. Singeliweza kufanya chochote kujiokowa mwenyewe au wewe kujiokowa mwenyewe. Ni yale Kristo aliyo tufanyia sisi katika Mungu au yale Mungu alitufanyia katika Kristo. Ona? Si eti vema kama naweza hivi au natenda hivi, ni kama yeye alifanya hayo.

Vema sasa, sisi tuko ndani yake ndio Yeye alistamili hukumu ya Mungu; Yeye alichukuwa hukumu ile. (Isaya 63:3). Naye hana hatia ya dhambi, hakutenda dhambi, bali alifanywa dhambi kwa ajili yetu (2korinto 5:21). Kwa hiyo mradi tu umo katika Kristo, uko huru kwa hukumu “Nionapo damu, nitapita juu yenu. (Kutoka 12:13). Ona, Ona? Naam. Damu, ndiyo inayo waweka ninyi huru.

Sasa mwenye dhambi hana budi kusimama hukumuni na hakutakuwepo hukumu ila hii ni kama tu mviringo au upinde wa mvua wa damu ya Yesu Kristo ikizunguka mradi tu umo ndani humu... kama Mungu angetazama dunia katika hali yake usiku huu kwa njia nyingine yoyote isipokuwa kwa damu ya Yesu Kristo yeye angaliuagamiza katika muda wa sekunde moja. Yeye angepaswa kufanya hivyo. Bila shaka angaliuagamiza hapo ndipo hukumu inakuja.

Sasa, kama- au mradi tu mwanadamu yuko huku duniani. Haijalishi kama mtu yule ni mlevi na mcheza kamari, na mwenye dhambi wa kuongofya rehema za Mungu bado zinamfanyia upatanisho. Na mwanamke, huenda akawa, vyovyote awezavyo kuwa, kahaba ama chochote kile, damu ya Yesu Kristo ingali inamfanyia upatanisho, lakini mara nafsi yake inapoondoka katika mwili huu naye aenda ng'ambo yake, amepita rehema na kuingia hukumuni. Mngu amekwisha kumhukumu amekwisha kuhukumiwa.

Unajihukumu mwenyewe kulingana na vile unavyochukua ule upatanisho wa Mungu kwa ajili ya dhambi zako, Ona? Jihukumu mwenyewe humuoni yeye kama atosha kukusamehe wewe. Ona? Kama wadhani Yeye atakusamehe, ungama makosa yako, naye atakusamehe.

Ndipo kwa Roho mmoja (tazama) sisi sote tumebatizwa mwili, mmoja. (1 korintho 12:30) Na kama vile mwili huo ulivyofunuliwa na Mungu. Ulifufuka toka kwa wafu ukahesabiwa haki, umeketi kwa mkono wake wa kuume katika nguvu na mamlaka mbinguni. Kwa hivyo hao waliokufa katika Kristo, wamo katika Kristo na huru kwa hukumu, na watakuja katika huo ufufuo. (Ufunuo 20:6, 1 korintho 15:51-54).

Sasa. Lakini tukifa sasa- tukifa sasa, tunaenda moja kwa moja katika uwepo wa mwenyezi Mungu katika mwili wa kimbinguni. Kama ningemkuta vile vile juu kule, sisi sote tukifa sasa. Saa moja tangu ningesema salamu. Ndugu Neville niongee naye.

Tazama Yesu aliwaambia Wanafunzi wake, walipokuwa na Ushirika wao, akasema. Sitakunywa tena uzao wa mzabibu hata siku ile nitakapokunywa mpya pamoja nanyi katika Ufalme wa Baba yangu. (Matayo 26:29)

“sivyo ona? Naam, kwa hiyo wanapokufa.... mtu aliyehesabiwa haki anaposimama katika uwepo wa Mungu huingia katika uwepo wake kama kiumbe asiyekufa na kuishi mazingira yalio barikiwa ya amani hadi siku ile ambayo- atakaporudi tena (1 wathesalonike 4:16)

Sasa, kulikuwa na wakati ambao watu hawakuingia katika uwepo wa Mungu walipokufa, wale waliotakaswa. Hiyo ilikuwa katika haki Agano la kale. Wao walienda katika mahali paitwapo paradiso, nazo nafasi za wenye haki ziliongojea humo katika paradiso lakini paradiso palikuwa mahali ambapo Mungu aliweka hizo nafsi kama katika nchi ya ndoto, hata damu ya Yesu Kristo ilipomwagika; kwa maana damu ya mafahali na mbuzi na haingeondoa dhambi, ilifunika tu dhambi, damu ya Yesu huondoa dhambi, (waefeso 1:7; Yohana 1:29).

Mwatambua kuwa – Yeye alipokufa pale kalvari... na Yeye aliporudi aliwafufua toka kaburini wale watakatifu waliokufa chini ya kule kutakaswa kwa damu ya mafahali na mbuzi na ndama. Nao wakaingia katika huo mji (lo!) na kuwatokea wengi (Matayo 27:51-53) Picha nzuri jinsi gani, jamani laiti tungeipaka rangi kwa muda mchache mtazame Yesu alipokufa.

Hapo kama msemavyo mara nyingi, naamini, kanisani humu, kunaorodha kama, ndani humu mnaishi viumbe vinavyokufa. Na kila mmoja yumo katika kusanyiko hili kubwa la hatia, la weusi na giza. Watu wanaokufa huishi ndani humu sasa, au wao huvutwa na ushawishi toka U- upande huu, au toka upande ule hawezi kuwa hapa kiumbe wa Roho mwenye dhambi au Mtakatifu, bila kushawishiwa toka kuzimuni au toka Mbinguni (Ezekieli 37:17-24). Kama unashawishiwa toka hapa. Unatoka juu, mwili wako wa kimbinguni unakungoza juu hapa lakini kama umuovu na mnafiki, na mtu asiye jali mwili wako wa kimbinguni uko chini hapa, haijalishi unawaza vipi uko kule juu; kwa sababu tunda uzaalo mbele ya watu lathibitisha unakotoka kwa hiyo uko hapa jinsi ulivyo mahali pengine maisha yako unayoishi hapa yanaonyesha tu urithi wako ulivyo uondokapo hapa je wafahamu?

Sisi hivi sasa tu (lo, ninapowaza hilo) hivi sasa tumetukuzwa katika uwepo wa Mungu. Tu waamini waliozaliwa mara ya pili “kwa maana nyumba ya maskani haya iliyo ya duniani hii ikiharibika, tuna mengine yanayongoja utukufuni, “(11 5:1-4) si mahali penginepo, ng'ambo kule tayari ya kungojea sasa. Na miili ya dunia hii inaukuwa kuvikwa hiyo isiyo kufa. (Warumi 8:20-23). Siyo? Magonjwa na maumivu na kuvunjika moyo, na maumivu ya moyo na ... Eel. Nitafurahi nyumba hii yenye masumbuko itakapofungwa. Nanyi, je? Naam, Bwana! Tunaweza kuenda nyumbani. Naam.

Tuna- ugua tupate kuvikwa, Roho anaugua Ee, utazamapo na kuona maumivu haya yote yametuzunguka, mikusanyiko yote, uvundo, na dhambi, na maisha yanayo kufa, na uongo, na kila kitu, nadhani, Ee umebaki muda gani’’?’?

Hivi karibuni nitahubiri mahubiri yangu ya mwisho. Nitaiweka Biblia yangu chini hivi na kuenda nyumbani. Ee. Utakuwa wakati jinsi gani. Na maskini haya ya kiisha hapa, haitachukuwa hata sekunde moja kufika yale kule ng’ambo hata nawe pia. Jamani!

Sasa, huko ni wapi? Tutaupata lini? Sasa! “wale waliohesabiwa haki, hao pia aliwatukuza” (Warumi 8:30). Na je, mnajua ya kwamba miili yetu iliyotukuzwa na isiyokufa inatungoja katika uwepo wa Yesu Kristo sasa hivi, inatungoja sisi tuje?

Je, mwajua mtoto mchanga azaliwapo duniani humu, kabla hajazaliwa yuna uzima lakini hajazaliwa bado. Na mara tu mtoto huyu ajapo a-a anapoanza ku- kuzaliwa mapafu yake yamefungana, ni maiti misuli tu yake inatetemeka na kutikisika-tikisika. Lakini jambo la kwanza, kugongwa tu kidogo kumoja kuwili hivyo, na atapata pumzi yake kuna nini? Mara tu huo mwili wa kawaida uanzapo kuumbika katika mama, kuna mwili wa kiroho unaungoja kumpokea mara tu huyo mtoto mchanga azaliwapo.

Na bila shaka kama vile kuna mwili huu wa kiroho unaozaliwa, kuna mwili wa kawaida unaungoja kupokea mara tu- unapoondoka ulimwenguni humu, Ona? Na kadhalika kurudi tena Edeni, kurudi moja kwa moja.

Kwanini, mauti, hilo tu-hilo linatupilia mbali uchungu wote wa mauti uliopo. Nasi ajabu Paulo angesimama na kusema, “U wapi Ewe mauti, mauti uchungu wako? Ku wapi ewe kaburi kushinda kwako? Yeye alisema “Lakini Mungu na ashukuriwe atupae kushinda kwa Bwana wetu Yesu Kristo (1 korintho 15:57). Naam, marafiki! Nyumba ya maskani haya iliyo ya dunia ikiharibika tayari tunayo mengine yanayongoja kwa hivyo sahau hayo.

Sasa. Kwako, rafiki, kama wewe uliyeuliza hili ni mwenye dhambi, Mungu akurehemu Naam, Bwana! Hauko tu chini ya hukumu sasa, si hapa, la utafanikiwa na kuendelea. Na hayo yote ni kwa rehema za Mungu kwamba ufanikiwe na kufanya ufanyavyo. Hilo ni kweli lakini hivi karibuni, kama wewe umwenye dhambi na nafsi yako iponyoke. Itaingia hukumuni na itahukumwiwa ndiposa, utatupiliwa mbali na utakuwa katika mateso hata utakaporudishwa duniani humu tena (Yohana 5:28-29). Na utapokea mwili usiokufa, mwili usiokufa ambao hauwezi kufa, na utatupiliwa mbali katika gaza la nje ambapo kutakuwa na kilio., kuomboleza nakusaga meno (Marko 9:3-44). Na utateswa katika nyakati zote zijazo Yesu alisema hayo. Hiyo ni picha nyeusi lakini ndiyo Biblia isemavyo.

Kama Mungu alihukumu dhambi hivyo na iligharimu gharama kuu kama hiyo, itakuwaje kama rohohao wachafu wataachiwa tena? Tungekuwa na jambo lingine kama tumekwisha kuwa kuwa nalo katika miaka elfu sita iliyopita. Sivyo? Hakuna kuwa na nafasi tena.

Sasa, unasema. “Vema, naamini. Kuwa unapoingia kaburini u- unaenda kuzimuni,” Mwili wako unaenda kuzimuni, naam. Kuzimuni maana yake ni utengano. Mauti maana yake ni utengano “mwili wako hapa, unakufa, unatenganishwa. Unatengana na wapendwa wako hapa, lakini hayo sio tunayo sio tunayo nena. “Na kama vile watu wanavyowekewa kufa mara moja na baada ya kufa hukumu. (Waebrania 9:27).

Kwa hivyo mwamini anapokufa, yeye huenda katika uwepo wa muumba wake, Mungu wake. Na mwenye dhambi anapokufa yeye huenda kwa kituo chake. (Zaburi 9:17, Ezekieli 31:12). Ndipo katika kule kurudi... sasa, naongea sasa kuhusu walio wateule.

Lakini kunawengi watakao-fufuka katika ufufuo wa pili, ambao watasimama hukumuni na wenye dhambi, wahukumiwe pamoja naye. Nataka ni hakikishe mnafahamu hilo. (Ufunuo 20:4-6).

La kwanza litakalotukia ni ku-kuja kwa Bibi-Arusi. Kutakuwa na watu ulimwenguni... mimi huenda ukatofautiana na hili kidogo, lakini sikiza kwa sababu tu kwamba ulimpokea Kristo kama Mwokozi binafsi, hilo si kusema kuwa utanyakuliwa. Kutakuwa na masalio watakaopitia katika yale mateso na ile dhiki iliyo kuu. (Ufunuo 12:15-17: Ufunuo 7:13-17). Kanisa litatwaliwa kwa kunyakuliwa, (1 wathesalonike 4:13-17).

Bila shaka tunapo kufa, kama tuko katika Kristo Yesu tunaenda juu kuwa na huu mwili mkuu kule ng’ambo, Yesu Kristo, kama sisi tuwenye dhambi, tunaenda kuwa na kundi kuu la wasioamini; na Mungu alisema sehemu yetu ilikuwa pamoja na wanafiki na wengineo, kuzimu (Ufunuo 21:8). Amina.

Sikiliza kile “Malaki 4” Imesema kuhusu viwango: sasa tujapo tunakumbuka kuwa twaishi hapa katika viwango vitatu. Na sijui kama ninaweza kuvitaja au la. Kimoja ni Nuru, na kingine ni Vitu. Sasa nuru, vitu na wakati na zile hisi zetu tano huwasiliana na hivyo viwango. Kuona kwetu huwasiliana na nuru, kugusa kwetu huwasiliana na vitu, na kadhalika.

Sasa, lakini tuna uwasiliano wa sayansi, kile kiwango cha nne, kama ilivyo. Kwasababu zikipitia papa hapa jengoni sasa zaja picha, sauti za radio, picha za televisheni, ambazo hisi zetu haziwasiliani nazo walakini wana bo-bomba au kioo kinachoyachukua hayo mawimbi ya hewa

nyepesi sana na kuyadhihirisha. sasa.hivyo, mwaona, mumu humu jengoni mna, matendo ya watu yanayotendeka sasa hewani, sauti zinazo sikika sasa. Ziko hapa tunajua hivyo. Ni zakweli hasa. Na jambo likupasalo kufanya, wao- wao wanazinasa kwa... sielewi maarifa ya – ya vitu hivyo ambavyo sayansi imevumbua lakini twajua kuwa inatudhibitishia kuwa kiwango cha nne.

Sasa, kile kiwango cha tano ni ambapo wenye dhambi, asiye amini hufa na kwenda kule kiwango cha tano ni, vema kiwango cha kuogopa. Sasa mtu huyu... Na Mkristo anapokufa huingia katika kiwango cha sita kisha Mungu yuko katika kiwango cha saba. Sasa basi mwaona, Mkristo anapokufa yeye huenda chini ya Madhabahu ya Mungu moja kwa moja hadi katika uwepo wa Mungu chini ya Madhabahu. Na yeye anastarehe.

Kuifafanua mtu awapo na jinamizi, yeye huwi amelala kabisa, wala hawi macho yeye yuko katikati ya usingizi na kuwa macho na hiyo ndio humfanya yeye kutetemeka na kupiga mayowe ya kuogopa, kwa sababu yeye hayuko usingizini. Wala si macho na ukichukua hilo laonyesha mtu aendako akifa kabla hajaondoka. Yeye tayari amemaliza wakati wake, amesha kufa duniani naye hawezi kwenda katika uwepo wa Mungu, kwa sababu hafai kwenda kule bila ile damu. Naye amenaswa wakati wake duniani umekwisha. Naye amenaswa katikati, na yuko katika jinamizi. Mwaona? Yeye hawezi kurudi, kuja duniani kwa sababu wakati wake umekwish. Yeye yuko katika jinamizi, na ataishi hivyo hadi siku ya hukumu. Jambo la kuogopa kuwa ndani yake.

Katika wakati wa kufa, nimewasikia watu walipojua ya kwamba walikuwa wanakufa na vitu walivyoweka siri maishani mwao katika hali ya kukata tamaa walikuwa wanajaribu kuyakiri. Unaona? Na kujaribu kuchukuwa jambo hili na ulisahihisha, nenda, tafadhali nenda, lifanye, “Unaona, katika kukata tamaa walipaswa kuwa wamefanya jambo hilo hapa kabla, unaona. Si kungojea mpaka wakati wa dharura, “je! Utanifanyia kadha-na kadha”? Dharura husababisha kukata tamaa wakati tunapaswa kufanya jambo hilo bila dharura.

Basi, si hoja unani. Mwanamke, Mwanaume, Mvulana ama Msichana yeyote uliye Mkristo si Mkristo, muhudumu. Shemasi yoyote uliye, iwapo utaamini tu kwa moyo wako wote kwa muda mdogo tu, na kufanya haya usiku wa leo kumfanya Mungu ajue ya kwamba u mwaminifu. “Mungu...” Sasa tazama mimi ni mpendekoste. “Unasema”. “Mimi ni hiki,” ama chochote ulicho. Ninakiri kucheza katika roho lakini Ndugu Branhamu nilidhani mradi tu tulifanya hivyo, tumepata, Hamna.

Kama unaniamini mimi kuwa nabii wa Mungu, sikilizeni maneno yangu. Huu ndio udanganyifu wa siku hizi. Biblia haikusema zingefanana sasa hata zingewadanganya walio wateule kama ingewezekana (matayo 24:24) walio wateule ndani ya nafsi.

Bali kama ulicheza katika Roho, na ungali una mambo ya duniani, mna walakini kama unanena na lugha: Paulo alisema waweza kunena kwa lugha za wanadamu na za Malaika na hata sijaokolewa,” (1 korintho 13:1-3, Matayo 7:21-23). A-haa, aina zote mbili. “naweza kufurahi sana, naweza kuwa na Imani, naweza kuhubiri Injili naweza kutoa mali yangu yote nikiwalisha maskini, naweza kupeleka neno la Umishenari kote Ulimwenguni, na bado si kitu mimi,” Mnaona? Nikile kilicho ndani cha upande wa ndani, ndugu. Roho yako huondoka unapokufa, inaruka, bali nafsi yako inaendelea kuishi. (Muhubiri 12:5-7).

Hivyo kifo kiko chini ya utawala wetu kupitia Yesu Kristo, ambaye alishinda kifo, kuzimu, kaburini, magonjwa huzuni, kila kitu kingine alishinda yote (11 Timotheo 1:9-10). Na sasa tumefufuka pamoja naye, tukikaa katika ulimwengu wa Roho. (Waefeso 2:4-6). Kuzungumzia kiroho, katika Kristo Yesu na vitu vyote chini ya miguu yetu. Hata ufufuo mwili uko chini ya miguu yetu, sababu tuko ndani yana Kristo. Je unalipata hilo? Mradi tu umelipata hilo hiyo ni vema sasa, liweke tu katika mawazo yako. Unaona? Tumepita kutoka mautini kuingia uzimani. Kimwili, kiroho, kila hali na kila kitu, na vitu vyote ni mali yetu sasa (1 korintho 3:22-23).

Kifo si chochote; tumekipata; ni chetu hakiwezi kunitawala; na-kitawala. Jinsi gani? Kupitia yeye aliyenifanya mshindi. Sababu tayari nimeshinda kifo. Namna gani imefanya hilo? Kumwamini Yeye. Unaona? Kifo kiko katika dhambi, kutokuamini. Mimi sio asiye amini, mimi ni mwamini nimeinuliwa kutoka kitu hicho, nimefufuliwa. Na ninakupata kikamilifu kwangu kote kimwili na ufufuo wa kiroho, kila kitu (Waefeso 1:13-14, 1 korintho 1:2-22).

Hakuna jambo lingine linaloweza kutendeka kwa mtu yeyote kubwa hivyo. Kama kumbadilisha kutoka mautini kuingia uzimani (Yohana 5:2:20). Kama ulikuwa katika kufa, kimwili Yeye angekuponya mwili, hilo ingekuwa jambo kubwa sana, bali hakuna jambo kubwa sana. Bali hakuna jambo kubwa kama aliyekuwa mfu kiroho na Mungu akamrudisha akiwa hai. (Waefeso 2:1-5). Jamani. Watu. Je umetowa taarifa ya kuwekewa nafasi kimbele kwa ajili ya kubadilisha vazi? Je umefanya matayarisho ya kuwekewa nafasi?

Huwezi kuingia pasipo kufanya hivyo na kuzungumza nanyi kwa lugha ya kisasa. Bali mwafahamu, kama ukienda Hotelini na kusema, “Vema, nina..” je ulikwisha toa taarifa ya kuwekewa nafasi? Vema, samahani, kila kitu kimejaa uko nje katika baridi. Kwasababu ulishindwa kutoa taarifa. Hakuta-kuwa na mtu yoyote pale kukutana nawe. Utapaswa kwenda nje huko katika giza la milele ambapo kutakuwa na kupiga makelele na kilio, na maombolezo, na kusaga meno lazima; lazima huwezi kuingia mji huo (Ufufunuo 21:1-27). Una kwa sababu hukutoa taarifa. Lazima uwe nayo ili uingie katika mji huu ambapo Yesu amekwenda kuandaa mahali kwa ajili yako. Kumbuka huna budi kuwa na taarifa, na vazi la wokovu umelivaa.

NUKUU

“Mambo yatakayokuwepo”-par 22-24-ujumbe wa kiingereza muhubiri wasita Uk 457 para 281.

“Maswali na majibu (mwaka wa 10-2-51) sehemu ya pili swali namba 61 uk 234 para377

“mwaswali na majibu(mwaka 54-01-03)swali namba 15,para 24-47-52

Kiwango cha sasa cha huduma yangu

Uk 5 para 21-23-25

Kukata tamaa

Uk 11 para 46

Uongozi

Uk 43 para 316-319

Njia ya nabii wa kweli

Uk 10-kiingereza

Mungu aliye mwingi wa rehema uk6 para-37

jiwe la kiroho la kujengea na 120 kutoka kwenye Neno lililofunuliwa la saa hii, iliyokusanywa na Gerd Rodewald Friedenstr. 69 D – 75328 Schomberg, Germany (+49) 72357613 Fax : (+49) 72353306. www.biblebelievers.de

Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itaizunguka dunia na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyochaguliwa kimbele imesikia.

(Ndugu Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk 724)

Kwa nakala zaidi kiingereza, Kiswahili andika kwa

Charles E. Kanju

Box 553 Korogwe – Tanga

Cell phone: 0784 704299/ 0718230098

Email: chaelika@live.com.